TANGAZO LA SERIKALI NA. 1036 la tarehe 13/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA MISECHELA KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA MISECHELA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Misechela kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Misechela ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa kwenye Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Misechela.

Madhumuni yatangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Taifa Misechela ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu ya uwanda wa chini, nyasi, miti ya miombo na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi

kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au maneo ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Taifa Misechela.

Uwasilishaji wapingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu Misechela kuwa Msitu wa Hifadhi ya Taifa Misechela, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

---

JEDWALI

---


*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA TUNDURU

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA MISECHELA

Makadirio ya eneo: Hekta 12220.91 au Kilometa za Mraba 122.21 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Misechela unaopatikana Wilaya ya Tunduru katika Mkoa wa Ruvuma kama lilivyochorwa upya katika Ramani ya Idara ya Upimaji Na. Jb 3160 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo




GPS Survey,Surveyed by Gasper D. Vicent 2022

Dodoma
11 November, 202

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*